Vivyo Hivyo Nuru Yenu na Iangaze Mbele ya Watu

Nimeshtukia jambo hili tu kama vile nanyi mlivyolishtukia. Nilishuka nikaja . . . Sina budi kuungama kwamba nimetenda kama mnafiki. Nilikuja nimechelewa kidogo tu. Nilidhani, "Ndugu Neville atakuwa anahubiri nitakapofika kule, kwa hiyo hatanisemesha neno lo lote. Ataendelea moja kwa moja."

2 Nilipoingia mlangoni, Billy akaniambia, akasema, "Ndugu Neville tayari anahubiri. Umewahi vizuri tu."

Nikasema, "Sawa."

3 Akanijia, akasema, "Bado sijaanza kuhubiri. Nilikuwa kwa namna fulani nangojea."

4 Kwa hiyo nikawazia, "Vema, labda . . . " Nikasema, "Ninajua jinsi ilivyo kuhubiri, mara mbili ama tatu kwa siku, kwa namna fulani inakuchosha." Tunajua jambo hilo. Hasa sana watu wakiwa ni vijana kama tulivyo sisi, unajua, miongoni mwa hao vijana ambao—ambao hawachukui muda mrefu. Kwa hiyo kwa namna fulani tuko pamoja, kama ndugu, na kwa namna fulani tunashikamana pamoja, na mioyo yetu pamoja, mawazo yetu pamoja, tuweze kufanya kazi pamoja, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

5 Nasi tunapenda kuwa pamoja na ninyi. Ni—ni jambo zuri sana. Kwa hiyo nilimwomba tu Bwana anipe fungu dogo tu pale, cho chote kile, nipate kuanza kwa namna fulani. Bado sijui nitakalosema, lakini tutaanza tu, na ndipo basi ko kote atakakotuongoza. Ni kweli ya kwamba tunaninii . . .

6 Nilipaswa kuanza mkutano wa siku sita huko Fairbanks, Alaska, tarehe kumi na tano, kuanzia tarehe kumi na tano. Lakini sidhani nitaweza kufika huko kwenye wakati huu, kwa sababu nina mkutano mwingine nitakaouendea, huko British Columbia. Kwa hiyo sidhani nitaweza kwenda huko wakati huu. Pia, wao wanataka kutayarisha mkutano wa wafanyi biashara, Wanaume Wafanyi Biashara Wakristo.

7 Kwa kweli ninaomba na ninataka sana maombi yenu kuhusu mikutano inayokuja ambayo tunajaribu kutayarisha kwa sasa. Nami nilipata mwaliko, siku chache zilizopita, wa kitu fulani kilichoonekana kizuri kwangu. Nami sijui kama ni Bwana aliye katika jambo hilo, ama siye. Itanibidi tu ningojee na kupata kujua. Wafanyi biashara walinitaka nije Phoenix, mnamo Januari, na niende kwenye kila kanisa, usiku mmoja, kote katika

jiji la Phoenix, kisha nifanye mkutano baadaye. Kwa namna fulani hilo lilionekana linapendeza, kwangu mimi, kwa maana lingenipa na—nafasi mimi ya kupata kuzungumza na makanisa na wahudumu wote.

8 Kwa kawaida, watu hufikiri, wanapokuwa karibu nami, ati kwa sababu ninayakemea sana madhehebu, ya kwamba ninawachukia watu walio kwenye madhehebu. Sivyo nilivyo, hata kidogo.Ninawapenda.

9 Ni kama tu vile ningalimwona mtu akishuka mtoni hapa katika mtumbwi, na mtumbwi huo ulikuwa umetobokatoboka sana, nami nilijua hivyo, na nilijua mtumbwi huo haungeweza kamwe kuyavuka mawimbi yale kule chini. Ningekuwa nikipiga mayowe na kuushutumu mtumbwi huo, kwa nguvu sana niwezavyo, lakini si huyo mtu aliye ndani ya ule mtumbwi. Ninalaumu mtumbwi huo. Ninajua huo mtumbwi hautamaliza safari. Pia ninajua madhehebu hayatamaliza safari. Lakini ninajua watu waliomo mle ndani watafaulu, kama tu mtu ukitoka humo. Unaona?

10 Lakini ni kama vile mtu ungalikuwa na gari kuu kuu na ulikuwa unapanda mlima, nami nilijua wakati ulipoanza kuteremka upande wa pili hukuwa na breki. Mimi nisingekuwa na kitu dhidi ya mtu huyo, ninayapigia makelele. Si yeye. Ni lile gari alilopanda. Ataumia.

11 Na hivyo ndivyo ilivyo kuhusu madhehebu. Ninafikiri watu wanaoshikilia madhehebu hayo, kana kwamba yalikuwa ni Mungu Mwenyewe, nao wanaliacha Neno la Mungu, wapate tu kushikilia madhehebu. Vema, wanapofanya jambo hilo, ninasikitika watafanya kosa baya sana. Na si kwamba mimi nina jambo lo lote dhidi ya mtu huyo, bali ni huo mtumbwi aliopanda, unaona, nina hakika hatamaliza safari. Madhehebu hayatafaulu kamwe, bali Kristo atafaulu. Kwa hiyo toka tu kwenye—kwenye huo mtumbwi unaovuja wa umadhehebu, uingie kwenye Meli ya salama ya Sayuni, ile Meli ya kale ambayo bado haijashindwa kamwe kutua pwani mapema, Kristo.

12 Na hiyo ni kusema, nafikiri, ingenipa mimi nafasi, nipate kuzungumza na watu hao.

13 Sasa, nilifikiri, labda . . . Usiku wa leo, ni usiku wa ushirika. Nami ninasikia wamekuwa na ubatizo, watakuwa na mwingine. Ningetaka kushuka nije kwa—kwa ajili ya ushirika. Niliukosa wakati uliopita, kwa kutokuwa hapa. Niliukosa. Na nilijua hii ilikuwa ndiyo Jumapili ya kwanza, kwa hiyo nilijitayarisha kuwapo hapa, ili kwamba nipate kuwa kwenye ushirika usiku wa leo.

14 Kwa kuwa hakika ninafikiri ya kwamba ni jukumu la kila Mkristo kushiriki Meza ya Bwana. Biblia ilisema, "Msipoula huu, hamna shirika Nami." Nami ninaamini ya kwamba ni wakati wa ku—kuonyesha mtu alivyo kwa Wakristo. Kama

hatushiriki, hatuna shirika Naye. Na kama tukiushiriki, isivyostahili, basi tuna hatia ya Mwili na mauti ya Kristo. Kwa hiyo inafikia mahali ambapo inamfanya Mkristo aombe kinaganaga, anapokuja kwenye Meza ya Bwana. Tunapaswa kuja kwa kicho, kwa makini, kwa heshima sana, tukija, tukikiri makosa yetu yote, tukiombeana. Si hivyo tu, bali inatupasa kuhisi . . . Kama kuna ndugu au dada miongoni mwetu, ambaye tunajisikia kidogo amekosea, mioyo yetu inapaswa kuwa na mzigo kwa ajili ya mtu huyo kwenye usiku wa Meza ya Bwana, hasa sana, kuwaona, kwamba wataweza kuja na kushiriki Meza ya Bwana, wasije wakahukumiwa pamoja na ulimwengu. Kwa sababu, wao ni ndugu zetu na dada zetu.

15 Sasa, kwa majuma machache yaliyopita, mawili au matatu, majuma mawili, yanaelekea kuwa matatu, sijazungumza sana. Nimekuwa nikipumzika tu. Kwa maana kwa namna fulani huu ni msimu wangu mfupi wa kupumzika, kabla ya ule—ule msukumo mkubwa.

16 Nilikuwa nikimsikia Ndugu Neville akizungumza juu ya ubashiri huu miongoni mwa wanasiasa na watu ambao kweli wana ufahamu wa mambo hayo, kuhusu vita vya atomiki vinavyokaribia sana, vingedumu kutoka Desemba mpaka Januari. Vema, ni niniii tu . . . Hiyo karibu ni kweli. Wangevitangaza, waviazishe, na halafu mabomu mawili matatu, na hilo lingemalizia mambo. Kwa hiyo taifa hili haliwezi kustahimili vita vya atomiki. Tusingeweza kabisa kustahimili. Lakini hilo halimshitushi Mkristo, ama hangalipaswa kumshitua Mkristo. Tunapaswa kuwa tayari dakika yo yote, tukimngojea Bwana wetu aje. Na, loo, mara nyingi, unaona, haya . . .

17 Haya hayarekodiwi, haya ni ya hapa nyumbani tu. Hakuna kanda, kwa hiyo haikulazimu kuchunga unayosema, kuhusu kumwendea mtu mwingine, ama kitu kama hicho. Ni watu wa nyumbani tu.

18 Hebu niwaambie kitu nilichokuwa nikifanya. Nimekuwa nikiwinda kuchakulo. Na, lakini, sikuwa nimefanikiwa vizuri sana. Hakuna kuchakulo wengi sana. Na ninaelekea Alaska sasa, kuwinda kondoo.

19 Na pengine watu fulani wanaweza, watu wengi, huwezi kusema jambo hilo kwenye kanda ama cho chote kile, kwa maana kuna watu wengi wanaopinga kuwinda, hata kidogo. Na, lakini, daima niliona, ndio hao hao wanaopinga kuwinda, hebu waletee tu kipande cha nyama, watakifurahia mno, unaona.

20 Na kama vile yule bibi, wakati mmoja, alivyoniambia. Alisema, "Ndugu Branham, unataka kuniambia ya kwamba— ya kwamba unawinda sungura?"

21 Nikasema, "Ndio, mama." Sasa, mimi sizungumzii juu ya mtu huyo wa thamani. Ameaga dunia.

22 Na kwa hiyo akasema, "Loo, hilo ni jambo la aibu. Hupaswi kuwapiga risasi hao sungura." Kwa hiyo, basi, haikuwa . . . Msimu huo hata haukwisha ikawa bibi yuyo huyo aliposema, "Naomba uniletee sungura wachache?" Akasema, "Hivyo ndivyo vitu vitamu sana nilivyopata kula."

Nikasema, "Vema, nafikiri huo ndio ninaoita 'utamaduni.'" Unaona?

Na mtu fulani akasema, "Una maana gani?"

23 Nikasema, "Bibi huyo ana utamaduni." Nikasema, "Utamaduni ni mtu fulani asiye na ujasiri wa kutosha kumwua sungura, bali anaweza kumla baada ya mtu mwingine kumwua. Kwa hiyo nafikiri huo ndio—huo ndio ungeuita 'utamaduni.'" Loo, mimi . . . Mimi sininii . . .

24 Mimi ni mhifadhi. Siamini katika kuua na kuharibu vitu ovyo. Ninamfundisha mvulana wangu, hao wanaowinda pamoja nami, "Kamwe usiue kitu cho chote isipokuwa iwe uko tayari kukila." Unaona? Kiache. Usiue ndege kwa shabaha tu. Unaona? Hilo si sawa. Chukua dango, liweke huko nje na ulipige risasi. Ukitaka kula mnyama pori, basi, aliwekwa huko kwa kusudi hilo. Na kumwua bila sababu, ni kama kuharibu bure kitu cho chote kile. Si haki kufanya jambo hilo, kuwaua wanyama kwa—kwa kusudi la kupiga shabaha.

25 Na wakati ninapoenda huko milimani, marafiki zangu, si sana sana napandisha huko "kwenda kuwinda." Ninaenda huko nipate kuwa peke yangu na Mungu. Baadhi yenu, kama mtachunguza, matukio yangu makuu kuliko yote niliyo nayo, ni wakati niko huko nikiwinda, wakati ninapokutana na Mungu.

26 Kati ya matukio yangu yote, sijapata kamwe kuwa na moja kama nililopata hivi majuzi asubuhi, papa hapa, nikienda kuwinda kuchakulo. Nimeona mambo mengi maishani mwangu, ishara na maajabu, na kadhalika. Lakini hilo lilinigusa kwa nguvu zaidi kuliko cho chote nilichowahi kupata hadi sasa. Hebu wazia tu sasa, karibu tu na mapambazuko, kunanyesha, mawingu mazito kote kote, nami naona pinde tatu za mvua, zimesimama mbele yangu, zikipanda, kutoka kwenye kitu kama kikombe kilichokaa juu ya kilima, ziko pale zikipanda juu zaidi na zaidi, mpaka unashikwa na ganzi mwili mzima mpaka mtu inakuwa ni vigumu kuzungumza. Kisha unasogea karibu Nazo, basi unamsikia Yeye akinena na kuthibitisha Ujumbe ule ule unaohubiri, kwamba ni Kweli. Unaona?

27 Kasema, "Yesu wa Agano Jipya ndiye Yehova wa la Kale. Yeye alibadilisha tu utaji Wake." Vema, niliketi, nikisoma jambo hilo. Nakuta, neno lilo hilo, ambapo Yeye "alibadilisha sura yake," katika Kiyunani, lilimaanisha, "alibadilisha kinyago Chake." Kwa kweli si *utaji* Wake, bali "kinyago" Chake. Ilifikia mahali Yeye "aligeuka," unaona, hiyo inamaanisha Yeye "alibadilisha njia Yake." Yeye alikuwa ni Mungu, Yehovah.

Na Mungu, Yehova, alijigeuza Mwenyewe kwa Roho akawa Mwanadamu. Yeye ni Yehova Mungu yeye yule. Ambapo, *huyo* alikuwa ni Baba, na *huyu* ni Mwana, akiwa ni Mtu yule yule.

28 Na ni vipi, basi, Yeye alinipa jambo fulani la kuzungumzia. Ikiwa Bwana anapenda, ninakusudia kuwako kwenye mti ule ule, asubuhi, mnamo mapambazuko. Nami na—natumaini atanitokea tena. Na—natumaini kwamba Yeye atanitokea, ili kwamba niweze kujua la kufanya. Nina mzigo moyoni mwangu kwa ajili ya watu. Ninapoona ile saa ikikaribia na ninajua ya kwamba watu hawako tayari, na wapendwa wangu, sijui nifanye nini au niseme nini. Nitapanda kule nione kile Yeye atakachoniambia. Kwa hiyo iweni katika maombi kwa ajili yangu.

29 Kisha nitaondoka, kesho alasiri ama Jumanne asubuhi. Mimi, pamoja na Ndugu fulani hapa kanisani, tunaondoka kwenda British Columbia. Nami ninaenda huko pamoja na ku—kundi la wahudumu wa Kipentekoste. Imedhaminiwa, hiyo ziara. Hainigharimu hata senti. Nao walidhamini ziara hiyo na wakachukua kiongozi. Na huyo kiongozi ni ndugu wa Kipentekoste aliyejazwa na Roho Mtakatifu. Na halafu nilipata watu wachache wa kubatiza katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo, watega wanyama fulani na—na mambo kadha wa kadha wakati nikiwa niko kule, watega wanyama wa Norway na kadhalika, ambao wameninii, kwa njia ya hizi kanda ambazo zimesambazwa, wameona Nuru, nao wanataka niwabatize katika Jina la Yesu Kristo.

30 Naye kiongozi wa Shirika la Wahudumu wa British Columbia, yanibidi nikutane naye Jumapili ijayo jioni katika Loji ya Pine huko Dawson Creek, British Columbia. Naye anaona njaa na kiu ya kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo.

31 Kwa hiyo, unaona, kwa jumla si kuwinda, marafiki zangu. Ninataka kumbatiza kiongozi huyu, na kila mhubiri anayeambatana nami wakati huu, katika Jina la Yesu Kristo. Ninyi niombeeni. Mnaona? Ambapo, ninajua ni kweli, inafanya moyo wangu kuona njaa na kiu ya kumwona Mungu.

32 Sasa, kabla hatujaliendea Neno, sitachukua muda wenu mwingi sana, nitafundisha kidogo tu kutoka kwenye Maandiko fulani, mpaka tunapoweza kufikia mahali, tuone ambapo tunaweza kuanza kuomba. Na kupata . . .

33 Ninaamini mtu fulani anasimama hapa. [Ndugu Branham anatulia wakati mtu fulani anapozungumza kutoka kwenye kusanyiko—Mh.] Mimi—mimi, samahani, je! mtu aliye karibu kidogo alisema jambo hilo? Sikusikia tu vile huyo ndugu . . . [Mtu fulani anasema, “Anataka umweke wakfu mtoto wake.”] Ati nimweke wakfu mtoto wake? Bila shaka, ndugu yangu. Naam, bwana. Mlete mtoto wako moja kwa moja hapa. Tutafurahi kufanya jambo hilo.

34 Na, sasa, ni—ninaamini jambo hili. Sasa, ili kwamba nipate kulieleza kwa watu kabla hawajaja.

35 Je! Ndugu Arnold yuko ndani? Teddy? [Ndugu fulani anasema, "Ndiyo."—Mh.] Vema. Tafadhali njoo utupigie piano.

36 Sasa, watu wengi huwanyunyizia watoto hawa wachanga, nao wanauita huo ni ubatizo wa watoto wachanga. Sasa, kama kanisa lako linafanya jambo hilo, hilo, hilo ni sawa. Bali, unaona, kama wakifanya hivyo, ni kanuni ya kanisa. Si Andiko. Andiko haliungi mkono kubatiza kwenu kwa kunyunyi-. . .

37 Andiko haliungi mkono kunyunyizia, kwa jinsi yo yote. Hakuna mtu aliyewahi kunyunyiziwa, katika Biblia. Wao walikuwa, kila mtu, alibatizwa kwa kuzamishwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo.

38 Lakini, sasa, mtoto mchanga, katika Biblia, waliwaleta na kuwaweka wakfu kwa Bwana. Waliwaleta watoto wadogo na kuwaweka wakfu kwa Bwana, wakawaweka kwenye mikono ya Bwana Yesu.

39 Ni sawa, dada, mlete mtoto wako. Na wengine wo wote, walio na watoto wao wachanga, ambao wanataka wawekwe wakfu, mbona, tutafurahi kufanya jambo hilo, kufanya ibada ya kuweka wakfu kwa ajili ya watoto wetu wachanga. Sasa, Yesu, katika Maandiko, ninii . . .

40 Sasa, katika kanisa hapa, tuna mchanganyiko wa madhehebu ya kila aina. Baadhi yao, Protestanti, baadhi ya Wakatoliki, na hata tuna Wayahudi ambao wamekuja hapa, hao ni Wayahudi wa Kiothodoksi. Hiyo ndiyo sababu tunajiita kabisa "wa madhehebu mbalimbali ."

41 Na sasa, ili kwamba mpate kufahamu, tunajaribu, kwenye—kwenye kanisa hili, kuwa kanisa la Kimaandiko, tukidumu tu na Biblia. Po pote Biblia inaposema jambo lo lote, tunafuata hilo vivyo hivyo hasa. Sasa, kanisa la kwanza, na Wakristo wote pamoja nanyi wahudumu mtakubali ya kwamba Hii ni historia ya Kanisa la kwanza. Sote tunajua jambo hilo. Hivi ndivyo ilivyotukia hasa.

42 Nilikuwa nikizungumza na kasisi mmoja, kasisi Mkatoliki anayeishi juu hapa mtaanii, hivi majuzi. Naye alisema, "Bw. Branham," kasema, "wewe ni mtu a—asiye Mkatoliki ama ni Mprotestanti?"

Nikasema, "Mprotestanti."

Akasema, "Basi unatupinga."

43 Nikasema, "La, bwana. Mimi siwapingi—siwapingi hao watu, ni hilo—hilo kanisa, fundisho la kanisa hilo."

Akasema, "Hivi wewe, basi, je! unajiita Mbatisti ama Mpresbiteri?"

Nikasema, "La, bwana. Ni Mkristo tu."

44 Ndipo akasema, "Vema, umeundia fundisho lako wapi? Ili uwe Mkristo, huna budi kuwa na msingi wa kuunda fundisho fulani."

Nikasema, "Hiyo ni kweli." Nikasema, "Ni Biblia."

"Vema," akasema, "Hiyo ni historia ya kanisa Katoliki."

Ndipo nikasema, "Vema, ndiyo kusema kwamba wale mitume walikuwa ni wakatoliki?"

Akasema, "Naam, bwana."

45 Nikasema, "Vema. Nitakubali ya kwamba hilo ni kweli."

Yeye . . . Nikasema, "Basi kwa nini ninyi pia msidumu basi na Maandiko?"

46 Akasema, "Unaona, Kristo alilipa kanisa nguvu za kuyabadilisha Maandiko wakati wo wote wanapotaka."

47 "Vema," nikasema, "Basi mmeyabadilisha, na kupata kile mlicho nacho leo?"

Akasema, "Naam, bwana."

48 Nikasema, "Basi, ninataka kuuliza jambo fulani. Basi hapana budi Kristo hafurahishwi Nalo, kwa sababu Yeye alimwaga Roho Mtakatifu juu ya Kanisa la kwanza. Waliponya wagonjwa, na kufufua wafu, na kutoa pepo, na kufanya miujiza mikubwa mno, chini ya Fundisho la Kanisa la kwanza la katoliki. Na jambo hilo halijaonekana katika kanisa Katoliki tangu walipobadilisha Fundisho hilo."

49 Sasa, hebu na turudi nyuma tuwe wakatoliki asilia. Hebu na turudi nyuma tuwe kile Biblia ilichosema wao walikuwa. Kristo alitembea pamoja nao. Hiyo ndiyo sababu, marafiki zangu, tunajaribu kutohukumu kanisa lo lote, watu walio makanisani, bali tunajaribu kuliweka tu kama Biblia ilivyosema.

50 Sasa, katika Biblia, hapajawahi kuwako na mtoto mchanga aliyebatizwa. Kamwe hapajawahi kuwako na mtoto mchanga aliyenyunyiziwa maji, mahali po pote katika Biblia. Lakini hapa ndipo lilipo katika Biblia, kasema, "Wakawaleta watoto wachanga kwa Yesu, apate kuweka mikono Yake juu yao na kuwabariki." Ndipo Yeye akasema, "Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, wala msiwazuie, kwa maana walio mfano wa hao Ufalme wa Mungu ni wao." Sasa hilo ni kweli kabisa. Sasa, kwa hiyo, sisi huwaleta watoto wadogo na tunawakabidhi kwa Baba wa Mbinguni, kutoka kwenye mikono ya mama, ama baba, na kuwatoa wakawekwe wakfu, kwa uaminifu wote.

51 Watoto wangu, ninao wawili, bado, ambao bado hawajabatizwa, kwa maana ndiyo kwanza wawekwe wakfu. Nina mtoto mchanga Utukufuni, ambaye aliwekwa wakfu tu, hakubatizwa.

52 Kwa sababu, ubatizo ni kwa ajili ya ondoleo la dhambi, unaona, kuonyesha ya kwamba wewe umetubu. Mtoto huyo

mchanga hajafanya jambo lo lote la kutubia. Ni mtoto mchanga, ndiyo kwanza tu azaliwe hapa ulimwenguni. Hana nguvu za kujia hapa, unaona, na wala hana dhambi. Kristo alipokufa Msalabani, alikufa apate kuondoa dhambi ya ulimwengu. Mpaka mtoto huyu mchanga atakapofanya jambo fulani la kutubia, Damu ya Yesu Kristo inamfanyia upatanisho.

53 Lakini sasa mama na baba, wazazi, wana haki ya kumleta huyo mtoto mdogo, na kumtoa kwa Mungu, huyo mtoto mchanga waliyepewa na Mungu.

54 Hana kule hekaluni. Aliahidi. Alikuwa ni tasa. Alikuwa ni mzee. Hakuwa na watoto. Aliomba kwa bidii sana madhabahuni, mpaka kuhani akatoka na akamlaumu kwamba amelewa. Alikuwa akipiga makelele na kulia, madhabahuni, kusudi Mungu ampe mtoto. Ndipo akasema, "Mungu, kama utanipa mtoto, nitamrudisha moja kwa moja mahali hapa na kumkabidhi Kwako."

55 Enyi akina mama, hivyo ndivyo mlivyopata mtoto wenu. Mungu alikupa mtoto wako. Ni kama tu vile alivyompa Hana mtoto wake. Na sasa mnawarudisha watoto wenu wachanga usiku wa leo, hekaluni, kama tu vile Hana alivyomfanyia mtoto Samweli, pia, katika ibada ya kuwekwa wakfu. Sasa, tunamweka wakfu na kumrudisha mtoto wako, kwa maombi, kwa Mungu Ambaye alikupa wewe mtoto. Nami ninaomba ya kwamba wavulana hawa wadogo na wasichana wanaosimama hapa usiku wa leo, watakuwa ni manabii wa kiume na wa kike kama Samweli, wa kale alivyokuwa, kwa Bwana, ambaye mnamrudishia.

Sasa, kama wasikilizaji watainamisha vichwa vyao kwa muda kidogo tu.

56 Mungu mpendwa sana na mwenye rehema, tunakikaribia kiti Chako cha neema na rehema, saa hii, kwa ajili ya kizazi kinachokuja baada ya sisi kuondoka. Jamaa hawa wadogo wanaosimama, nao wana—wanawashikilia. Wameshikilia, usiku wa leo, katika mikono ya mama na baba zao. Wao ndio mbegu ya jamii ya kesho. Ili wawe na uhakika ya kwamba wao wamepata mwanzo sahihi, mama hawa na baba wanawaleta hawa watoto wadogo hapa wapate kuwekwa wakfu, wapate kuyatoa maisha yao ya uchanga kwa Mungu aliye hai.

57 Baba, mimi pamoja na mchungaji tunasogea hapa mbele, na kuwatoa watoto hawa Kwako katika maombi ya kuweka wakfu. Wabariki, Baba yetu. Tunaomba ya kwamba utawabariki, wawe watumishi Wako wadogo. Jalia waishi maisha marefu, yenye furaha hapa duniani, na waone Kuja kwa Bwana Yesu. Si hivyo tu, jalia waishi maisha marefu, yenye afya, ya furaha, na wawe watumishi Wako. Naomba uwaongoze. Naomba upate wahubiri, waimbaji, wainjilisti, wamishenari, kwa ajili ya kesho, kutoka kwa watoto hawa, kama kuna kesho ijayo. Tujalie,

Bwana. Tutawaweka wakfu Kwako vizuri tujuavyo, kulingana na Maandiko Yako ambayo Wewe umetuachia, Neno Takatifu.

58 Ambalo, limeandikwa katika Kitabu cha mwisho cha Biblia, "Mungu atamwondoa kutoka katika Kitabu cha Uzima, mtu yule atakayeondoa Neno moja kutoka katika Hiki, ama kuongeza neno moja Kwalo." Tunatambua, basi, Biblia hiyo ni Neno takatifu la Mungu. Nasi hatuwezi kuongeza jambo moja Kwayo, wala kuondoa jambo moja Kwayo. Kwa hiyo, Bwana, tunaliacha tu jinsi Wewe ulivyolikabidhi, na kulifundisha, na kujaribu kuliishi, kwa neema Yako.

59 Wakati, tunapowaweka wakfu watoto hawa, kama walivyowaleta kwa Yesu katika siku zilizopita. Kama Yeye angalikuwa hapa duniani usiku wa leo, katika umbo la mwili, hawa akina mama na baba wangekimbilia miguuni Mwake, na kuwaleta hao watoto wadogo. Naye angeweka mikono Yake juu yao na kuwabariki. Wewe umeketi katika mkono wa kuume wa ukuu huko Juu, usiku wa leo, Bwana Yesu. Nasi tumeachwa hapa, kama mtumishi Wako. Tutaweka mikono yetu juu yao, kufanya maombi Kwako, ili kwamba uyachukue maisha haya machanga na uwatumie kwa utukufu Wako. Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba. Amina.

Waleteni. [Mpiga piano anaanza kupiga *Waleteni*—Mh.]

60 Una mtoto mdogo? Jina lake ni nani? John. Jina la mwisho, dada? [Mama anasema, "Meyer."—Mh.] Meyer. Loo! Huyu ni mtoto John Meyer, mtoto mdogo ambaye sisi sote tumemwombea, hivi majuzi. Huyu hapa, pamoja nasi, usiku wa leo.

Na tuinamishe kichwa chetu.

61 Bwana Yesu, wakati mimi pamoja na mchungaji Wako tunaposimama pamoja, usiku wa leo, tukichukua kutoka katika mikono ya mama huyu mtoto huyu mchanga, wakati baba yake akiangalia. Kwa matarajio makubwa kwa ajili ya mtoto huyu mchanga, katika siku zajazo. Sasa namtoa mtoto huyu John Meyer Kwako, Bwana, kwa ajili ya utumishi Wako. Katika Jina la Yesu Kristo, tunamweka wakfu kwa Mungu. Amina.

62 Mungu akubariki. Mungu ambariki mtoto huyo mdogo. Mumdumishe mwenye furaha, awe ninii . . .?. . .

63 Hatimaye, amefika. Ninafikiri ulimpata mtoto huyu mdogo karibu wakati ule ule, bali mimi sikujua hilo. Jina lake ni nani? [Mama yake anasema, "Elizabeth Collins."—Mh.] Elizabeth Collins. Vema. Ninamjua babaye; angemwangusha. Ninajua jambo hilo. Unaona? Lakini mtoto Elizabeth Collins.

Na tuinamishe kichwa chetu.

64 Baba wa Mbinguni, mfanye huyu Hana mwingine mdogo. Mfanye mtumishi kwa Bwana. Mbariki. Mbariki baba yake na mama yake, nyu—nyumbani mwao. Na jalia aishi kwa ajili ya

utukufu wa Mungu. Tujalie, Bwana. Tunakutolea, Elizabeth Collins, katika kuwekwa wakfu kwa maisha yake. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki.

65 Sijui kama unaweza kuinuliwa jukwaani? Unaweza? Jina lake ni nani? [Mama yake anasema, "Davonna Gayle Stayton."—Mh.] Davonna Gayle ["Stayton"] Stayton. Naam. Davonna Gayle.

66 Huyu ni mtoto Davonna Gayle Stayton. Mama yake na hao wengine wamekuwa wakija tu kanisani, wameninii... walimpokea Roho Mtakatifu, wakabatizwa.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

67 Baba yetu wa Mbinguni, tunapendezewa na ujasiri wa mama na baba hawa wadogo, kuja kwa mama huyu, jinsi alivyokuja, na maendeleo ambayo amefanya. Jinsi ambavyo Wewe umeibariki hii mioyo midogo myororo. Tunakupa Wewe kipenzi hiki kidogo, upate kuyabariki maisha yake machanga, Bwana. Na jalia awe mtumishi Wako. Wabariki baba na mama yake, pamoja. Jalia daima alelewe kwenye nyumba ya Kikristo, chini ya maonyo ya Mungu. Tunamtoa Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

68 Mungu akubariki, mtoto Davonna Stayton. Mungu akubariki, Ndugu Stayton.

69 U hali gani, wewe kitoto kidogo kipenzi? Unaweza kuja hapa, dakika moja? Ehee? Ningeweza...Wewe simama papa hapa, kipenzi, papa hapa. Jina lake ni nani, ndugu? [Huyo ndugu anasema, "Hannah."—Mh.] Ndugu Creech...Kuwa mdogo... Naam. Wewe ni mtoto Allen. Ana ufasaha wa lugha kweli, unaona. Vema, huyu—huyu ni mtoto Hannah Creech. Labda angeniruhusu kumwinua juu. Yeye ni msichana mdogo mzuri sana.

Na tuinamishe kichwa chetu.

70 Baba wa Mbinguni, tunakupa mtoto huyu mchanga, aliye sasa kwenye miguu ya mamaye. Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba Wewe utambariki na kuyafanya maisha yawe chombo kitakachotumika katika Ufalme Wako. Mbariki baba yake na mama yake. Jalia mtoto huyo alelewe katika nyumba ya Kikristo, kwenye maonyo ya Mungu. Tunaweka mikono yetu juu yake na kumweka wakfu Kwako, maisha yake machanga, kwa utumishi Wako. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Awabariki, asubuhi ya leo. Awabariki!

71 Je! yeye haji? Jina ni nani? Ati nini? Don? ["Don...?... Benjamin."] Benjamin. Benjamin. ["Sawa. Mtoto Benjamin."] Huyu ni Benjamin...?...["Hiyo ni kweli."] Ndugu mdogo na dada.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

72 Baba yetu wa Mbinguni, tunapokupa Wewe kitoto hiki kipenzi, ingawa bado ni kichanga sana, Bwana, kujua yale yanayoendelea. Bali Wewe unajua mambo yote. Tunaomba ya kwamba utayabariki maisha yake ya utotoni, Bwana. Bariki nyumbani kwake. Na, Bwana, jalia jamaa huyu mdogo aishi kwa utukufu wa Mungu, maisha mazuri, marefu na yenye furaha; kama ikiwezekana, aone kule Kuja kwa Bwana Yesu. Tujalie hayo, Bwana. Tunamweka wakfu Kwako, kwa utumishi Wako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

73 Na huyo alikuwa ni. . . [Mtu fulani anasema, "Mvulana."—Mh.] Huyo ni jamaa mdogo mzuri sana. Unaona? Benjamin. . .?. . .Jamani, huyu ni mvulana mkubwa jinsi gani! Jamani! . . .?. . .Loo, jamani!

74 Sasa, angalia. Mtoto huyo anamwangalia kwa makini sana. Nimekuwa nikimbeba. Jina? [Baba yake anasema, "William Davis."—Mh.] . . .?. . .Mtoto William Davis. Hakika ni katoto kazuri sana, kweli, kamesimama karibu na jamaa huyu mdogo.

Na tuinamishe kichwa chetu.

75 Bwana Yesu, tunakupa Wewe, mvulana huyu mdogo wa thamani, kwa utumishi Wako. Mama yake na baba yake wamemleta, Bwana, apate kutumiwa kwa utukufu wa Mungu. Sasa, kwa hiyo, Bwana, tulipokuwa tunasoma kutoka kwenye siku zilizopita, Yeye aliweka mikono Yake juu ya watoto wachanga kama huyu na akawabariki. Mikono yetu ni uwakilishi mbaya wa Yake. Bali tunaomba katika Jina Lake, na kukupa mtoto huyu mchanga, kwa ajili ya maisha ya utumishi, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Akubariki! [Baba anasema, "Akubariki, mchungaji."—Mh.]

76 Bibi Bowers. . .?. . .Ati, kipenzi, jina lako ni nani? Loo, jamani! [Mtu fulani anasema, "Sussie. Sussie ana jina."—Mh.] Angalia kama ana jina. Nitafurahi kukushika. Wewe ni mvulana mdogo mzuri. Sussie Bate kadogo.

Na tuinamishe kichwa chetu.

77 Baba wa Mbinguni, msichana huyu mdogo mwenye macho maangavu. . .?. . .Bila kujua ni kitu gani kilichoko huko mbele; hakuna hata mmoja wetu anayejua. Lakini, baba na mama, wanamtaka akae katika njia iliyonyoka na iliyosonga. Na chombo kidogo kizuri namna hii, jinsi Shetani angetaka kukipondaponda. Bali wao walimleta, kusudi Shetani apate kupigwa vita asimkaribie. Yafiche maisha yake machanga, Bwana, kwa utumishi Wako. Katika Jina la Yesu Kristo tunaomba. Amina.

Waleteni, waleteni,
Waleteni kutoka maeneo ya dhambi;
Waleteni, waleteni,
Waleteni watoto wadogo kwa Yesu.

78 Loo, jinsi . . . Hivi hamwuwapendi watoto wadogo? Kama watu hawawapendi watoto wadogo, kuna kasoro. Yesu alisema, "Msipoongoka na kuwa kama mmoja wa hawa watoto wadogo, hamtaingia kamwe katika Ufalme." Hata mmoja.

79 Baba fulani ana wasichana wawili wadogo kule nyuma, bado, aliotaka kuwaleta. Nilimwambia, "Walete moja kwa moja." Unaona?

80 "Tusipoongolewa na kuwa kama watoto hawa wadogo." Unajua nini? Ungeweza kudhuru maskini hisia zao. Baba na mama wanajua, mara nyingi wanaingia katika shida, wanawapiga. Mbona, mnamo dakika mbili, mikono yao midogo imekukumbatia moja kwa moja, na wamesahau mambo yote. Na hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya. Haidhuru ni nini kinachoendelea, hatuna budi kuwa wenye kusamehe na wenye kuhurumia, sisi kwa sisi, na—na—na kuwa namna hiyo, kama watoto wadogo, tulio tayari ku—kusamehe na kusahau, na—na kuwa namna hiyo. Hivyo ndivyo tu—tunavyopaswa kufanya. Na ndipo tunapofanya namna hiyo, tunaukaribia Ufalme wa Mungu basi.

81 Ninaamini wasichana wawili wadogo kwa namna fulani wana soni. Inawabidi Baba na mama wawasindikize waje nao. Vema, hilo ni sawa kabisa. Tunapenda tu jambo hilo. Tunapenda wasichana wenye soni. Ni nadra sana unaona mmoja anayeweza . . . Loo, hawa ni wale waimbaji wachanga. Sivyo? Huyu ndiye mmoja wa hao wanaoimba? Nilifikiria hivyo. Sawa, bwana.

82 Sasa, jina lako ni nani? [Msichana huyo anasema, "Ruth."—Mh.] Ruth. Hilo ni zuri sana. Ruth ni jina zuri sana. Ninalipenda, ninalipenda kweli kweli. Sasa, na jina hilo la mwisho ni jina gani? Ni . . . [Mtu fulani anasema, "Myers."] Myers, mtoto Ruth Mayers, yeye ni mmoja wa waimbaji wetu wachanga hapa. Je! ni mapacha? Inaonekana wanafanana sana, sivyo?

83 Baba yetu wa Mbinguni, tunakupa Wewe msichana huyu mdogo, ambaye baba na mama wanasema hawajawahi bado kuwaweka wakfu kwa njia yo yote kwa ajili ya utumishi na Ufalme wa Mungu. Tunaweka mikono juu ya mtoto Ruth, usiku wa leo, mtoto Ruth Mayers, na kuomba ya kwamba Nguvu za Mwenyezi Mungu, Ambaye amempa kipawa cha kuimba, ataendelea kumbariki. Na jalia maisha yake yawekwe wakfu Kwako, siku zote akiwa hapa duniani. Tunamkabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo.

84 Jina la huyo dada mdogo ni jina 0gani? Loyce? Vema, mtoto Loyce. Jamani!

85 Baba wa Mbinguni, tunaweka mikono juu ya mtoto Loyce, pia ana kipawa katika umri wake mdogo, kuimba Injili. Bariki vipawa vya watoto hawa, Bwana. Na sasa maisha yao yanawekwa wakfu Kwako, na wazazi wao. Hivi karibuni, Bwana, watakuwa ni wakubwa vya kutosha kubatizwa. Watakapoanza—watakapoanza kujua mabaya, na kadhalika, na kuanza kufanya makosa, ndipo hawana budi kutubu na kubatizwa. Mpaka wakati huo utakapofika, Bwana, tunawaweka wakfu Kwako. Jalia watumie vipawa vyao kwa utukufu Wako. Yatumie maisha yao, wakaishi maisha marefu, maisha yenye furaha, ya kukutumikia. Tunamweka wakfu msichana huyu mdogo Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

86 Mungu akubariki. Nenda, na Mungu na awe pamoja nawe, na akubariki daima katika kila kitu unachofanya.

Hilo ni sawa, Ndugu Neville.

Loo, ni—ninafikiri tu wao wanapendeza sana! Mimi . . .

87 Wasichana wangu wanakaribia kuwa watu wazima sasa, kwa hiyo kwa namna fulani sina budi kuninii . . . Nilikuwa nikiwabeba mgongoni. Lakini wao karibu wangeweza kunibeba mgongoni sasa, ni wa—wakubwa sana; hasa Becky, ni msichana mkubwa mzito.

88 Sasa hebu na tufungue Neno la Bwana, katika Mathayo 15 . . . ama mlango wa 5. Nasi tutasoma tu sehemu yake, ndipo nitatoa kutoka hapa, Bwana akipenda, somo dogo kwa muda wa kama dakika kumi na tano, ishirini. Kisha tutakuwa na Meza ya Bwana, na kutawadha miguu, na ibada ya ubatizo, vitatufikisha saa tatu u nusu hivi, basi, ama baadaye kidogo, kumalizia. Ningetaka kuanzia Mlango wa 5, kwenye kifungu cha 12.

> *Furahini, na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu.*
>
> *Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini chumvi ikiwa imeharibika itatiwa nini hata ikolee? Haifai* tena *kabisa, ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu.*
>
> *Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima.*
>
> *Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani.*
>
> *Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.*

89 Ningetaka kuchukua so—somo kutoka kwenye hicho kifungu cha mwisho hapo, ambacho ni kifungu cha 16: *Vivyo Hivyo Nuru Yenu na Iangaze Mbele ya Watu.* "Nuru yenu na iangaze vivyo

hivyo mbele za watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye Mbinguni."

90 Tunaona, katika Maandiko, ya kwamba kuna mahali pawili ambapo watu wawili mbalimbali wanazungumza juu ya kuhesabiwa haki. Na mmoja wao alikuwa ni Paulo, na huyo mwingine alikuwa ni Petro. Mtakatifu Paulo, na Mtakatifu Petro; na Paulo alikuwa akimhesabia haki Ibrahimu kwa imani, naye Petro alikuwa anamhesabia haki kwa matendo. Petro alisema ya kwamba alihesabiwa haki kwa matendo. Paulo alisema alihesabiwa haki kwa imani yake. Sasa, hawakuhitilafiana. Walikuwa wakiangalia jambo hilo katika mitazamo miwili mbalimbali. Na Paulo alikuwa akizungumza juu ya imani ya Ibrahimu, hiyo ndiyo Mungu aliyoona katika Ibrahimu. Naye Petro alikuwa akizungumzia kuhusu matendo yake yaliyonena juu ya imani yake. Kwa hiyo imeandikwa, "Nionyeshe matendo yako pasipo imani yako, nami nitakuonyesha matendo yangu kwa imani yangu." Sasa, kwa hiyo, Paulo, akiona kile kilichokuwa kinanenwa, na kile Mungu alichoona. Na Petro alikuwa akizungumza juu ya kile mwanadamu alichoona, na, maana, kama mtu ana imani, yeye atatenda kulingana na imani yake. Matendo yake yataionyesha kwa wengine.

91 Kwa hiyo ninaenda, ninataka kuzungumza juu ya jambo hilo, usiku wa leo, "Kuacha Nuru yetu iangaze."

92 Sasa, kwa dakika hizi chache tu, sitaki kuja hapa kusudi tu nipate kuonwa ama kusikiwa. Hilo lisingekuwa sawa. Lakini, labda, Mungu akinisaidia, labda tungeweza kuzungumza maneno machache hadi tufikie jambo ambalo litakuwa linatujenga, litakalotusaidia sisi sote, jinsi ambavyo tungeweza kuenda vizuri zaidi na kuishi maisha bora zaidi. Nina hakika hiyo ndiyo sababu ya sisi sote kuwapo hapa, ni kupata marekebisho na kupata ufahamu wa yale tunayoweza kufanya kutufanya Mkristo aliye bora zaidi. Kama nina jambo moja maishani mwangu ninalotumaini, ni kuwa Mkristo bora zaidi ya nilivyo. Nami nina hakika hicho ndicho kilio cha moyo wa kila mtu aliyepo hapa usiku wa leo, ni kuwa Mkristo bora zaidi.

93 Muda fulani uliopita, nilikuwa nikishuka kwenda barabarani, nikiwa ninaendesha gari kasi sana, na huku nikiangalia kama ninavyofanya kwa kawaida, nikiwa peke yangu, naendesha. Na ni safari ya upweke wakati unapoendesha ukiwa uko peke yako. Huwezi kufungulia redio, kusipokuwapo mtandao wa familia ambapo unaweza kupata muziki wa dini, kwa maana imejaa mchanganyiko wa mambo ambayo yangemtoa hata Roho aliye ndani yako.

94 Na po pote niendapo, baada ya mimi kuwa mzee kidogo, mbona, ninabeba pedi ndogo ya karatasi. Na wakati Mungu

anaponifunulia jambo fulani, ninaliandika tu. Na hata nimeandika kwenye tako la bunduki yangu, huko mwituni, kwa risasi. Na mambo kama hayo, kupata tu wazo fulani nililopewa. Ninachukua kibandiko kidogo kutoka kwenye nguo zangu, ama cho chote kile, na kuandika juu yake. Kitu kama hicho, nipate kuukumbuka Ujumbe huo.

95 Na nilipokuwa nikiendesha, kwenye barabara hii, niliona kibao kikubwa mno cha matangazo. Na kwa kawaida, unajua, wana vitu vingi sana vilivyobandikwa kwenye vibao hivi vya matangazo, bali mimi sikuona vitu kama hivyo kwenye ubao huu maalum. Kwa kawaida wana picha za—za wanawake walio nusu uchi, ama kitu kama hicho, wakitangaza aina fulani ya sigara, ama—ama wiski, ama pombe, ama kitu fulani, vibao hivyo vikubwa vinavyong'ara. Lakini nilishangaa, nilipotupa jicho kwa mara yangu ya kwanza, ubao mmoja ulinivutia, kwa maana haukuwa umechafuliwa na kitu cho chote kile. Haukuwa na uchafu. Ndipo nikaangalia nyuma, nione.

96 Ulikuwa ni ubao wa kuvutia. Nao umewekwa mahali pazuri, mahali ambapo tu, unapopiga kona hii, huyaepi matangazo hayo. Ndipo nikashangaa, ulikuwa na neno moja lilioandikwa juu yake, "Njaa?" Hilo tu, "Njaa?" Hilo tu ndilo lililokuwako. Halafu nikaona maandiko madogo sana chini ya huo ubao, yaliyosema, "Maili tatu mbele." "Njaa? Maili tatu mbele."

97 Vema, nikaanza kuchunguza jambo hilo. Hao watu hawakuwa sana. . . Kwa kawaida, kama wana mkahawa huko mbele, wao—wanashindana katika kuwashawishi watu; ile picha, steki kubwa zinazochachatika, na kadhalika. Na ukiingia, kwa kawaida hukuti kitu cho chote kama ilivyotangazwa, bali ni ta—tangazo tu. Lakini hili lilionekana kuwa na mtazamo tofauti.

98 Na tunajua ya kwamba siku tunayoishi leo, kuna faida ya kutangaza. Nasi tunaona, ya kwamba, watu hawa wanaofanikiwa sana katika biashara ni—ni watu hodari katika kutangaza. Wao—wao wanayatangaza kwenye televisheni. Wanayatandaza kwenye vibao, po pote wawezapo, kutangaza bidhaa zao. "Vuta sigara *hii*; hukohoi hata ukivuta gari nzima." Na, "Chunjio la mtu mwenye akili," na ushauri wa mtu mwingine, ama kitu kama hicho. Juu ya . . . na ninii . . . "Ishi kwa raha mstarehe, maisha marefu," kwa pombe yao. Na upuuzi wote kama huo, ni matangazo. Nao wanafutilia mbali kodi kubwa yao ya mapato, kwa matangazo tu. Na bila shaka yanaleta faida.

99 Kwa hiyo iwapo kuna faida, kufanya hivyo, nilianza kuwazia, "Basi kwa nini Ukristo usilete faida kama ukitangazwa?"

100 Vema, nikawaza, basi, "Ma—matangazo ni nini?" Huna budi kuwa na kitu fulani ambacho ni tofauti kidogo na kile walicho nacho wengine, ama kama ni kitu cha kawaida

sana, kama yalivyo mambo ya ulimwengu, hakitawavutia watu kamwe. Sasa, kama mtu angekuwa akitafuta gari, angelipita tangazo hilo. Lakini kama alikuwa na njaa, angekuwa akitafuta tangazo hilo.

101 Kwa hiyo ninaamini ya kwamba Mkristo ni ubao wa Mungu wa kuwekea matangazo. Ninaamini ya kwamba kila mmoja wetu sisi ni ubao wa Mungu wa matangazo. Na haitulazimu kupiga makelele sana juu yake, kama tunavyofanya. Ni kuishi tu maisha ambayo yatawafanya watu kuwa na njaa ya kuwa kama wewe.

102 Sasa, niliona kwenye ubao huu wa matangazo, ubao huu maalum, haukudai cho chote, hata kidogo, bali uliuliza tu swali, kama wewe una "Njaa?" Na huwezi kumwuzia mtu ye yote chakula cho chote wasipokuwa na njaa. Jambo la kwanza ambalo tangazo hilo linafanya, mtu anayepitia hapo hana budi kuliona.

103 Sasa, njia pekee ambayo ulimwengu utapata kumwona Kristo ni wakati mtu, watu, watakapomwona ndani yako na ndani yangu. Hiyo ndiyo njia watakayoweza kumwona Kristo. Dhamiri ya—yao imekufa isifahamu kutua kwa jua, mlio wa ndege, majani, na—na nyasi, na maua; na muziki, na Ujumbe na kadhalika, ambavyo tunafurahia baada ya kumpata Kristo. Lakini, mpaka tutakapofikia mahali ambapo tunamwonyesha Kristo wazi!

104 Sasa, kumbukeni jambo hilo. Kila mmoja wenu, tangu usiku huu na kuendelea, kumbukeni, ninyi ni vibao vya Mungu vya kuwekea matangazo. Nanyi—nanyi ni maajenti wa Mungu wa kutangazia. Sasa, ulimwengu utakutazama, waone kwamba Kristo ni kitu gani. Kwa hiyo hatutaki kupaka takataka chungu mbovu hapo, ambazo zinashuhudia kuhusu mambo ambayo kweli hayapo. Hebu kwanza tuwe hivyo. Ndipo basi tutakapokuwa hivyo, ndipo ulimwengu utakapomwona Kristo ndani yako na ndani yangu.

105 Jambo la kwanza, ambalo, tangazo lo lote, mtu hana budi alione.

106 Halafu, jambo lingine, hawana budi kulitaka. Sasa, kama wakiliona na hawalitaki, basi hilo ni jambo lingine. Lakini hujaweka tangazo la bure.

107 Bali kama wao, kwanza, wanapaswa kuliona, na halafu tunapaswa kulifanya la kuvutia sana kwao. Loo, natumaini tunaona jambo hilo, ule mvuto wa wokovu, jinsi unavyomfanyia mtu. Tunapaswa kuuvutia ulimwengu kwa Kristo. Na Injili kweli ina mvuto. Inao kwa wale walio na njaa ya Mungu. Inawavutia tu wale wanaoona na njaa na kiu, na hao ndio tunaowatafuta. "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu."

108 Lakini kuna wengi sana ambao Baba amewavuta, nao wanaona njaa na kiu ya kumpata Mungu, wala hawajui

watampata wapi, kwa sababu hao wanaopaswa kuwa ubao wa matangazo wamechafuliwa mno na mambo ya ulimwengu, hata hawawezi kuona ambapo wana zaidi ya walichokuwa nacho kabla hawajamjia Yeye. Wanaishi kama walimwengu. Wanazungumza kama walimwengu. Wanaimba nyimbo zile zile walimwengu wanazoimba. Wanavaa kama walimwengu, ninamaanisha, hasa sana kwa wanawake. Nao wanatenda kama walimwengu. Wanaenda mahali pa kilimwengu. Wanahudhuria burudani za kilimwengu.

109 Mtu fulani aliniambia, hivi majuzi, kuhusu mhudumu fulani. Nami ninampenda mtu huyo. Hapana shaka ila ni mtu mashuhuri. Yeye alisema, "Lakini alisema ya kwa—ya kwamba wewe ulikuwa ni hao watakatifu wanaojifingirisha," kwangu mimi, ya kwamba nilikuwa mtakatifu anayejifingirisha.

110 Nikasema, "Vema, si—si—dhani ndivyo nilivyo. Lakini," nikasema, "Ni—ninataka kuwa mtakatifu. Na kama Bwana akipata kuniambia nijifingirishe, nafikiri ningejifingirisha. Lakini na—nataka kuwa mtakatifu, hata hivyo, niishi maisha ya utakatifu, ninachomaanisha *u-safi* mbele za Mungu."

111 "Na kwa hiyo akasema, vema, ya kwamba unakimbia kwenda, kwenye nchi za ng'ambo, na kuzunguka hivyo, na ukajifanya mmishenari. Hakuna kanisa lililokutuma, nawe ulijifanya tu mmishenari kwa kujibunia."

112 "Vema," nikasema, "kama nilijifanya mmishenari wa kujibunia, jambo hilo halingeuvutia ulimwengu kamwe, kwa maana wao hawatafuti umishenari wa kujibunia. Wanamtafuta Kristo."

113 Na tunawaona, watu hao, wanaume hao na watu hao wanaofikiria mambo hayo.

Kuna tabaka mbili za watu. Mungu ana tabaka mbili mbali mbali.

114 Kuna watu ambao Mungu anawatumia kukaa nyumbani, na kufunga ndoa za wagonjwa, na kuzika wafu, na kubusu watoto wachanga, na kuwaoza vijana wao, na mambo kama hayo. Wengi wa watu hao hawajui jinsi ilivyo kubeba upanga, na kutoka huko nje na upanga ukatao kuwili katika mstari wa mbele. Hawajui vita ni nini, kupigana na adui. Wanatoka hapa nje, nao ni watu werevu, wanatheolojia, watu mashuhuri, wanaoweza kusimama, wakahubiri somo ambalo limepambwa sana, na pia wanaweza kuzungumza kwa msamiati mzuri sana, mpaka hata kamusi ya Webster ingeshindwa kujua walichokuwa wakisema. Wana digrii za chuoni, lakini hilo ni sawa wakati unapozungumza na kundi la wasomi linalotafuta tu kanisa la nyumbani.

115 Lakini ni hapo unapotoka kwenda huko nje kwenye mstari wa mbele vitani, ambako watu hao wana kitu cha zaidi ya hayo. Wanataka waone Nguvu za Mwenyezi Mungu zikidhihirishwa,

la sivyo hutaweza kuwashawishi. Wanataka kumwona Kristo katika kufufuka Kwake.

116 Hata hivyo, sasa, watu hao hawajui jinsi ilivyo kushika Upanga ukatao kuwili, kupigana ana kwa ana na adui kule. Ambako pepo na wachawi, cho chote kile, kinasimama pale, wachawi wanakupa changamoto kwa kila njia. Na ambako watu, wanaosoma Biblia hiyo, wanasema, "Kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, hebu nimwone Roho Mtakatifu akitenda kama alivyotenda hapo kale." Unaona? Ndipo huwezi kuchukua ki—kisomo na kufanya mambo hayo.

117 Inahitaji Nguvu na kufufuka kwa Yesu Kristo kudhihirisha hayo. Ndiyo. Na sasa hizo ndizo wananchi wenye njaa wanazotafuta. Ni lazima waziona, na inawapasa kuzihitaji.

118 Na hicho ndicho kitu kile kile taifa hili walicho nacho. Hiyo ndiyo sababu, usiku wa leo, kwamba tuna maonyo haya yote ya vita vya atomiki, ni kwa sababu mataifa yamekiona Hicho, taifa hili limekiona, wala halikitaki. Na hiyo ndiyo sababu hukumu ya Mungu iko juu yao. Ni kwa sababu tumepimwa katika mizani.

119 Niliona ambapo Rais wetu, Bw. Kennedy, Tom, alifikiri ndilo jina lake, Kennedy, ambaye aliwatuma hawa, maafisa kadha, huko kwenye vita hivi vya ubaguzi. Alituma huko mia nne na kitu, huko Kusini, kukomesha vita hivi vya ubaguzi. Na wakati alipofika mwisho, kwenye hesabu kamili, hawakutuma wengine, alikuwa na mia sita sitini na sita kamili. Hilo lilikuwa kwenye gazeti la *Time's*. Loo, laiti watu wangalikuwa wa kiroho, wangeweza kuamka na kuona "mia sita sitini na sita" ni kitu gani. Ndio hasa waliokuwa nao. Hayo yako kwenye toleo la *Time's* la mwezi huu.

120 Sasa, tunaona, ya kwamba, mpaka watu watakapoanza kumtaka Mungu, mpaka watu watakapoanza kuona kiu! Yesu alisema, "Heri wao walio na njaa na kiu ya haki, kwa maana watashiba." Sasa, inakubidi kuona njaa na kiu kwa ajili Yake.

Sisi ni vibao vya Kristo vya kuwekea matangazo.

121 Na Kristo ndiye mdhamini wetu, kwa kuwa udhamini huu unafanywa na Kristo. Naye anatupa Uzima wetu, tupate kumdhamini Yeye. Sasa, je! wewe ungekuwa ni mtu wa aina gani kama ulimdhamini mtu fulani? Tunapaswa kuwa tu watu wa aina gani kama sisi tume—tumedhaminiwa na Kristo? Yeye hutupa sisi wokovu. Hutupa uponyaji wetu. Hutupa afya na nguvu zetu. Hutupa chakula chetu. Hutupa makazi yetu. Basi, sisi tumedhaminiwa na Kristo. Na Wapentekoste, ambao wamejazwa na Roho Mtakatifu, ni wadhamini wa Yesu Kristo. Wamedhaminiwa na Yesu Kristo, na kupewa Roho Mtakatifu, wapate kuwa mfano kwa watu.

122 Tunapaswa kuwa nini, leo? Kanisa linapaswa kuwa wapi, leo? Tunapaswa kuwa ninii sana, katika hali fulani, ambalo ingeufanya ulimwengu wote uwe ukitaka kuwa kama sisi.

Kwa maana watu wanaenda mtaani na kusema, “Yule pale mtu, huenda nisikubaliane naye, juu ya Fundisho lake la dini. Lakini hebu niwaambie kitu kimoja, huyo ni Mkristo halisi.” Kunapaswa kuwe na wanawake wakipita mtaani, watu waseme, “Yeye anaweza akaonekana amepitwa na wakati. Huenda asiwe kama wanawake hawa wengine mnaowaona. Lakini kuna Mkristo mmoja humu mjini, kama yuko mmoja, ndiye yule kule anayeenda.” Kwa sababu, tunadhaminiwa na Yesu Kristo. Amina.

123 Loo, ni mtu wa aina gani tungepaswa, tunapaswa kuwa, kama sisi ni vibao Vyake vya kuwekea matangazo na tumedhaminiwa na Yeye? Basi, katika Kristo, Ndiye ambaye ndani Yake tunapata Uzima wetu, na tunapata nguvu zetu, na tunapata yote tuliyo nayo, vinatokana na Kristo. Yeye ndiye mdhamini wetu. Loo, nina shukrani sana kwa ajili ya jambo hilo!

124 Kwa hiyo, inatubidi tuwe kama Yeye. Na tuwe waangalifu kwa yale tufanyayo, yale tusemayo, yale tufanyayo katika maisha yetu ya kila siku, kwa maana tunadhaminiwa na Kristo. Tunapaswa kuenenda namna gani kama tumedhaminiwa na Kristo? Tunapaswa kusema nini kama tumedhaminiwa na Kristo? Kama mtu fulani ananena maovu juu yetu, tunapaswa kusema nini kama tunadhaminiwa na Kristo? Tunapaswa kuwa kama Kristo. Je! hiyo si ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

125 Sasa, sasa, kuna jambo moja tu. . . Na jambo lingine litupasalo kufanya, jambo moja tu, bali jambo lingine ambalo sisi wahudumu tunapaswa kufanya. Inatupasa kuhubiri Injili inayowavutia wenye njaa.

126 Sasa, kama tukihubiri Injili ya matakwa ya kijamii, na kusema ya kwamba, “Vema, unapaswa kuja na kujiunga na madhehebu yetu. Tulipata elfu nne na zaidi mwaka uliopita, katika madhehebu yetu.” Sio hilo. “Kama ukija kanisani kwangu, ama uwe mshirika wa kanisa langu, tutahakikisha ya kwamba unaangaliwa katika ninii. . . utakapozeeka. Na ukiwa mfuasi mzuri, ni kama hati ya bima, utatunzwa utakapokuwa mzee. Tutazingatia jambo hilo.” Huo ungali bado sio ule mvuto.

127 Jambo tunalotaka kufanya ni kuhubiri Injili inayouvutia ulimwengu wenye njaa.

128 Sasa, unawezaje kuwavutia walimwengu wenye njaa ambao hata hawataona mahali wanakotoka, kwamba wao ni nani na wanaelekea wapi, usipohubiri Injili inayomwinua Kristo katika mazingira yaliyo hai, papa hapa tulipo sasa hivi? Hatuwezi kulitekeleza hilo. Hakuna njia. Sisi, tungeweza kujiunga, tungeweza kujiunga na Masoni, Shi—Shirika la Watiri, ama shirika lo lote lile, kujiunga na shirika fulani ingekuwa ni sawa vile vile.

129 Lakini inatupasa kuhubiri Injili ambayo inawavutia watu wenye njaa, ambayo itawashika hao wenye njaa na kiu ya haki. "Heri wenye njaa na kiu ya haki, kwa maana watashibishwa." Sasa, watashibishwaje? "Wenye haki watashibishwa." Watashibishwa na kitu gani? Roho Mtakatifu.

130 Biblia ilisema, "Stefano alikuwa ni mtu aliyejaa..." Aliyejaa nini? Aliyejaa nguvu. Aliyejaa imani. Aliyejaa upendo. "Aliyejaa Roho Mtakatifu." Hilo ndilo lililomfanya alichokuwa, ni kwa sababu alijazwa na Roho Mtakatifu. Yeye alikuwa ni ubao halisi wa kumtangazia Kristo.

131 Wakati aliposimama pale, asubuhi hiyo, kwenye baraza la Wazee, nao wakamshtaki. Wakasema, "Mtu huyu," mambo yote aliyokuwa akifanya. Naye alisimama peke yake, ni yeye peke yake tu, hapo mbele ya baraza kuu la Wazee. Labda Wayahudi elfu mbili ama tatu, ama elfu tano, wakisimama pale wakimwelekezea kidole.

132 Biblia ilisema, wakati alitoka pale, ya kwamba, "Uso wake ulionekana kama wa Malaika." Hiyo haina maana kwamba alikuwa na Nuru iliyoangaza kutoka usoni mwake. Malaika angekuwa ni mjumbe aliyejua yale aliyokuwa akizungumzia. Stefano alitoka akaenda kule, pasipo kuogopa kufa. Hakuogopa kitu cho chote, kwa maana yeye alijua alichokuwa akizungumzia.

133 Kama vile Paulo alivyosema, "Ninajua Yeye niliyemwamini, na nimeshawishika ya kwamba anaweza kuweka kile ambacho nimemkabidhi."

134 Lakini Stefano alitoka akaenda kule, mbele ya baraza la wazee, kama kondoo miongoni mwa kundi la mbwa mwitu, walikuwa wakililia wayatwae maisha yake. Nao wakamshitaki, na kumshutumu. Yeye alifanya nini? Alisema, "Wanaume na ndugu, Mungu wa Utukufu alimtokea baba yetu, Ibrahimu, alipokuwa angali huko Mesopotamia, kabla hajaitwa atoke." Akaendelea na kuileta, historia yote ya Ibrahimu, na jinsi ambavyo kwa kupitia kwake angewaleta Wamtaifa. Na wakati alipofikia mahali fulani...Mwangalie, amejazwa Roho Mtakatifu. Wao, wakisubiri, hangengojea kamwe mpaka waweze kumtia mikononi mwao. Akasema, "Enyi wenye shingo ngumu, msiotahiriwa moyoni na maskioni, daima mnampinga Roho Mtakatifu. Kama baba zenu walivyofanya, ndivyo nanyi mnavyofanya." Yeye alikuwa ubao wa kuwekea matangazo ya Mungu.

135 Na wakati walipompiga mawe hata akafa, wakamtupa nje ya mji na kumpiga kwa mawe hata akafa, wakati alipokuwa anakufa, aliinua kichwa Chake Mbinguni na akawaombea msamaha wale waliokuwa wakimpiga mawe, kama vile Yesu alivyofanya msalabani.

136 Ndipo, Mungu aliona ubao wake mdogo wa kutangazia ukishushwa. Stefano akaangalia juu Mbinguni, kasema, "Tazama, ninaona mbingu zimefunguka, na Yesu amesimama mkono wa kulia wa Mungu." Ndipo akalala mauti mikononi mwa Mungu. Yeye alikuwa ni ubao wa matangazo kwa ulimwengu uliokuwa na njaa.

137 Unasema, "Vema, ni wangapi waliokuwa hapo? Ulisema kulikuwako na labda elfu tano. Ni wangapi wao waliookolewa?"

138 Kulikuwa na mmoja. Yeye hakukubali hilo kabisa papo hapo, bali miaka kadha baadaye. Haleluya! Mahali fulani, ushawishi wako haufi. Kulikuwa na mmoja aliyeshikilia koti, Sauli, yule kijana Mfarisayo aliyesimama pale, aliyeidhinisha na kushuhudia mauti yake. Lakini alipoona tangazo lile la Nguvu za Kristo aliyefufuka katika jamaa huyo mdogo, jambo hilo halikumwacha kamwe. Mtu yuyo huyo, Paulo, huyo aliyekuwa amesimama pale asubuhi hiyo, aliwaongoza maelfu ya watu kwa Kristo, kwa sababu mtu mmoja alikuwa yuko tayari kuyatoa maisha yake yawe ubao wa matangazo kwa ajili ya Yesu Kristo.

139 Tunapaswa kufanya nini leo hii? Haidhuru, haitubidi kuwa na wasikilizaji wengi. Haitulazimu kuhubiria watu elfu kumi. Hata haitubidi. Tunaweza kuwa ubao wa Mungu wa matangazo. Unajuaje kwamba maisha yako hayatamwingiza kijana fulani kwenye Injili? Baadhi yenu ninyi wazee, naona wanawake wazee, mnaweza kumwingiza kijana fulani huko nje kwenye huduma, ambaye angewavuta watu elfu kumi kwa Kristo, ni kwa sababu yeye alimwona Kristo ndani yako, kwamba ulimwonyesha Kristo dhahiri kwake, katika Nguvu rahisi ya Injili. Ndiyo.

140 Nafikiri tunamhitaji Kristo. Ndiyo, bwana. Njia pekee tunayomwona Kristo ni wakati ameakisi ndani ya sisi kwa sisi. Ninamwona Kristo ndani yako. Wewe unamwona ndani yangu. Hivyo ndivyo tunavyomwangalia Kristo. Ninakuja kwenye mkutano. Ninaanza kuhubiri. Ninawaangalia watu. Unaweza kuona kama wao wanavutiwa ama hawavutiwi, dakika chache tu. Unaangalia kwenye kusanyiko lako. Unaweza kujua kama unawachosha ama kama huwachoshi. Unaona? Na muda si muda unajua, unawaona wameketi pale, wakishikilia kila Neno, chini ya matarajio. Unaona? Ninamwona Kristo ameakisiwa katika mtu yule, kwa maana anasikia njaa na kiu ya Mungu.

141 Halafu, mimi, nikihubiri Injili, yeye anamwona Kristo akiakisi ndani yangu. Ninamwona Kristo akiakisiwa ndani yake. Hiyo inamaanisha Kristo yuko miongoni mwetu basi. Amina. "Kuona njaa na kiu." Ninawaangalia wasikilizaji, jinsi wanavyolichukua. Nasema kitu cho chote kile, ninaangalia lina matokeo ga—gani kwao. Ninaangalia nyuso zao zikichangamka, zimejaa furaha. Wako tayari wakati uo huo kupokea kitu fulani. Huyo ni Kristo. Ninamwona Kristo akiakisi katika mtu huyo

kwa maana Injili, hii Injili rahisi ya Kristo, inashikilia kwenye moyo huo, kwa kuwa wanaona njaa na kiu.

142 Nami nimeonyesha ubao wa matangazo hapa, tangazo moja. Ni tangazo la aina gani? Si kwa ajili ya theolojia fulani, si kwa ajili ya kanuni fulani ya imani ya kujibunia, bali ni kwa Kristo ambaye anaishi namna ile ile leo, na kwa ajili ya nguvu fulani, kwa kuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Amina. Hakika. Wanaweza kuona hizo nguvu za Mungu zikitenda kazi, wanaziangalia humo ndani ya majengo, na kumwona akiita watu, zikitambua siri za mioyo yao, zikiwaponya wagonjwa, zikifunua siri za mioyo yao, zikifungua maskio yasiyosikia, na zikiwafanya vipofu waone. Ni kitu gani? Ni kitu kinachovutia. Ni ubao wa Kristo wa matangazo. Na watu wanauona, nao wanakusanyika pamoja, na wanamtukuza Mungu. Ninamwangalia ndani yao wanapomtukuza Mungu. Wanamwangalia Yeye hapa, wakati zinapoelekea upande huu. Kwa hiyo, kupitia mmoja kwa mwingine, tunamwona Kristo akiakisi Nuru Yake. Sasa, haidhuru ninaweza kuiakisi jinsi gani *hapa,* asipoiakisi kwako, pia, kamwe hatutamfahamu Yeye.

143 Injili isingekuwa na nguvu pasipokuwako na mtu pale wa kuipokea. Kutakuwako na wengi ambao hawataipokea. Bali wale watakaoikubali, itaakisi ndani yao.

144 Labda kulikuwako na elfu tano asubuhi ile kwenye mauaji ya Stefano, bali kulikuwa na mmoja ambaye iliakisi ndani yake. Hata katika mwisho wa maisha yake, alisema, “Mimi sistahili hata kuitwa mmoja wa watakatifu,” alisema, “kwa maana nililiudhi Kanisa la Mungu, hata kufa.” Kukubali kwake katika kupigwa mawe kwa yule mfia imani, Stefano, hakukumwacha Paulo kamwe. Alisema, “Nililiudhi Kanisa, hata kufa.” Unaona? Hilo halikumtoka kamwe, kwa maana alimwona Kristo ameakisiwa.

145 Stefano alifanyaje jambo hilo? Yeye hakufanya miujiza yo yote, ingawaje yeye alijua ya kwamba Kristo alikuwa ni mfanya miujiza. Yeye alijua nguvu hizi zote na kadhalika. Lakini yeye alifanya nini? Aliyatoa tu maisha yake hivi kwamba wao waliona ya kwamba zilikuwa ni nguvu za Kristo. Amina.

146 Huenda usione ono kamwe. Huenda usiweke mikono yako juu ya mgonjwa, na kusikia nguvu za Mwenyezi Mungu zikimfanya mtu aliyekonda sana kupata uhai tena. Huenda usimwone Yeye kamwe amesimama kule katika pinde za mvua tatu ama nne. Huenda usipate kamwe kuona sura Yake. Huenda usisikie sauti Yake kamwe. Lakini bado unaweza kuwa ubao wa matangazo ambao utamwakisi Yesu Kristo, kwa maisha ambayo yamekuwa ni masafi sana na yasiyoghoshiwa na ulimwengu. Hayajachafuliwa na vitu vichafu katika maisha yako; lakini ni kitu kisafi, ambacho kitaufanya moyo wenye njaa kuona njaa na kiu upate kuwa kama wewe. Amina.

147 Ninyi ni chumvi ya ulimwengu. "Kama chumvi imepoteza ladha yake, itatiwa nini ikolee?" Hiyo ni kweli. Kuona njaa na kiu! "Nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuona matendo yenu mema, waone yale mnayofanya, na kumtukuza Baba aliye Mbinguni." Kuona njaa! Vibao vya matangazo! Kuakisi! ajabu! Ndiyo, bwana.

148 Sasa, pia, hatutaki kufanya jambo hili. Hatutaki kuliuza kwa haraka, kusema tu, "Vema, niliongoka jana usiku. Haleluya! Ulimwengu mzima . . . " Huwezi kufanya hivyo. Hayo ni mauzo ya haraka. Kama tukifanya hivyo, bidhaa hiyo si nzuri sana. Kama ukiishi tu vizuri, useme, "Ninajua wakati mmoja, ni—niliishi vizuri kwa majuma mawili baada ya kuongoka. Niliishi ninii mbili . . . Niliishi, majuma mawili, maisha makamilifu kabisa." Hayo ni mauzo ya haraka. Hiyo ni kama hii Hadicol tuliyokuwa nayo hivi karibuni, si kitu ila kibunda cha vitamini zilizofungashwa pamoja, wala haikudumu ila muda mfupi. Hatimaye ilikwisha.

149 Unataka kuwa Mkristo wa kila siku, Mkristo wa kila saa, Mkristo wa kila mwaka, si mauzo ya haraka. Lakini Nuru yako na iangaze vivyo hivyo.

150 Kama ukimwendea mtu fulani na kumwita ampokee Kristo, anakucheka usoni, usikasirike na kusema, "Vema, hakuna lo lote, la sivyo angeliikubali." La. Huko ni kuuza Hadicol. Sisi hatuuzi Hadicol.

151 Tunauza Injili, nguvu za Mungu aliye hai, Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Kama ulimwengu ulikuchukia, ulimchukia Kristo kabla haujakuchukia, kwa sababu ile ile iliyompeleka msalabani. Bali sisi ni wawakilishi Wake. Sisi ni vibao Vyake vya matangazo. Tunamtangaza Yeye.

152 Si lazima uwe na madoido, ninii nyingi, "Daktari, PhD, LLD! Kanisa kuu, lililotakaswa la *Fulani* na *Fulani*, lililoanzishwa huko nyuma kabisa katika *fulani* na *fulani*! Sisi tuna *fulani* na f*ulani*!"

153 Wewe wafanye tu waone njaa. Amina. Ubao rahisi, msafi wa matangazo ambapo Kristo ameandikwa kwenye maisha yako, "Ili kwamba watu wataona matendo yako mema na kumtukuza Baba aliye Mbinguni." Naam.

154 Usichafuliwe na takataka za ulimwengu. Usijaribu kujitangaza mwenyewe kama mtu fulani anayesema, "Vema, mimi ni mfuasi wa *Fulani*, hili kanisa kubwa. Ndilo kanisa lililo kubwa kuliko yote mjini humu."

155 Tuna mtu fulani karibu na kwetu huko, aliyeacha kanisa dogo hapa kwenye barabara kuu, aende kwenye kanisa kubwa, kwa sababu, wao walisema, "Tabaka bora ya watu walienda kule." Ati tabaka bora ya watu? Unaona? Wao hawajui. Akili za—zao zinaingia uchafu. Zimechafuliwa na mambo ya ulimwengu. Ati tabaka bora ya watu?

156 Tabaka nzuri ya watu ni nini? Watu waliozaliwa na Roho wa Mungu. Kama wao ni maskini sana hata hawajui mahali chakula chao kijacho kitatoka wapi. Hiyo ndiyo tabaka pekee ya watu iliyo na thamani. Hao ni watu waliozaliwa mara ya pili.

157 Wakati Yesu alipokuja, ilibidi achukue aina ya watu wa tabaka gani? Wasio na elimu, wavuvi, watu . . . Petro, mtume, yule mtakatifu mashuhuri aliyepewa funguo za Ufalme, hata hangeweza kuandika jina lake mwenyewe; aliyenuka samaki kutoka kwenye moshi wa siku nyingi zilizopita wa samaki na kadhalika, amevaa aproni yenye grisi. Yesu aliwachukua watu wa tabaka hiyo. Leo, wao wangemtoa kanisani kama akiingia, kweli, kuabudu. Unaona?

158 Watu wanaangalia "tabaka." Na je! unajua Ibilisi anaishi katika tabaka? Unajua ni nini kilichosababisha vita vya kwanza Mbinguni? Ni wakati ambapo Lusifa alianzisha tabaka kubwa zaidi ya watu, akachukua tabaka bora zaidi ya Malaika, akawazia. Ufalme mkubwa, mkubwa zaidi, ufalme maarufu zaidi, unaong'aa zaidi ya ule wa Mikaeli aliokuwa nao. Ndipo akafukuzwa Mbinguni. Unaona mahali tabaka inakotoka? Kaa mbali na tabaka.

159 Wenye njaa hawataki tabaka. Wenye njaa wanataka chakula. Ndiyo, bwana. Wanaosikia baridi wanahitaji moto, si picha, moto. Na wenye njaa, wanaoona kiu ya Mungu, wanahitaji Injili na nguvu za Yesu Kristo. Amina. Haidhuru ni rahisi jinsi gani, jinsi—jinsi isivyo- . . . jinsi isivyopendwa na ulimwengu, wao wanataka uhalisi wa mambo.

160 Mtu anayekufa, mtu anayejua hana budi kukutana na Mungu, hajali kuhusu tabaka yo yote. Yeye anataka kumwona Mungu. Anataka kupata uhakika, ili kwamba wakati atakaposhuka kuja mtoni, kutakuwako na mtu huko kumlaki na kumwonyesha njia. Anataka kitu fulani kinachomtia nanga sasa, kinachojua, "Ninajua Mkombozi wangu yu hai. Katika siku za mwisho, Yeye atasimama juu ya nchi."

161 "Nimeshawishika kwamba hakuna kitu kilichopo, kile kilicho siku za usoni, ama kitakachokuja, njaa, mashaka, ama cho chote kile, kinachoweza kututenganisha na upendo wa Mungu ulio katika Kristo." Hicho ndicho wanachotaka, wanataka kitu ambacho . . .

162 Si kivumba macho cha imani, kitu ambacho kinanunuliwa kwa haraka, "Na uje hapa na kujiunga na kanisa hili." Ninataka kitu ambacho . . . Unasema, "Vema, nitashuka niende kule na kujiunga na kanisa. Nitafanya ibada ya kuweka wakfu, mchungaji atanibatiza kisiri na kuniingiza kanisani." La, la. Hivyo sivyo. Hiyo ni moja ya bidhaa za kununuliwa haraka. Haitadumu muda mrefu.

163 Ninataka wongofu halisi wa mtindo wa kale, mwanamume ama mwanamke aliye tayari kutoka na kusema, "Nimekosea.

Ninataka kuwa kama jirani yangu. Ninatamani kuwa mwanamke kama jirani yangu. Ninataka kuwa mwanamume kama jirani yangu. Ninataka kutembea kitauwa sana mbele ya watu, hivi kwamba wataniwazia jinsi wanavyomwazia mwanamume yule. Ninataka kuwa kama Yesu Kristo."

164 Sasa, kumbukeni, katika kufunga, ni—ni—ninaendelea tu. Lakini, katika kufunga, ninataka kusema jambo hili. Sisi si wachuuzi Wake. Sisi ni Vibao vyake vya matangazo. Unaona? Usifikiri sisi ni wachuuzi Wake. Yeye hahitaji uchuuzi wo wote, anahitaji tu vibao vya kutangazia.

165 Nilikuwa nikifanya kazi kwenye Kampuni ya Utumishi wa Umma. Na hizi taa za Magol zikatokea. Walikuwa na shindano lake. Ye yote aliyeuza taa nyingi kuliko wote, alipata, loo, zawadi, na kadhalika, na asilimia fulani, waliyopata kwa kuziuza. Vema, kila mtu, kila mfanyakazi, ilibidi awe mwuzaji wa taa hizi. Vema, nikaanza kuwazia kitu kama hiki, "Kama bidhaa hii imedhaminiwa kwangu, kampuni imedhamini taa hii kwangu. Sasa, kama kwa vyo vyote taa hiyo inafaa, itajiuza yenyewe. Na kama haifai kitu, basi ninaweka kitu fulani kwa umma ambacho si kizuri."

166 Kamwe sijawahi kuamini jambo hilo. Siamini katika upuuzi huu wa wachuuzi wanaoshawishi sana. Hiyo ndiyo sababu mimi siamini katika dini. Kama nina bidhaa ambayo ni nzuri, itajiuza yenyewe. Hiyo ni kweli. Itajiuza yenyewe.

167 Kwa hiyo unajua vile nilivyofanya? Nilishuka kwenda kule, na nikamwambia yule msimamizi, nikasema, "Je! taa hizi zimedhaminiwa kabisa?"

"Zimedhaminiwa, kabisa."

"Hazitabadilika?"

"La, bwana."

168 "Na je! zimedhaminiwa? Usanii na kila kitu vimedhaminiwa?"

"Ndiyo."

169 Niliona zilitoa nuru nzuri nyororo. Mwanamke ye yote yule, angezifurahia chumbani. Unajua nilifanya nini? Nilibeba tu kama mia mbili za hizo, nami nikaanza kuzunguka kwenda kwa kila mtu niliyemjua hapa.

170 Kasema, "Unataka nini, asubuhi hii, Billy? Je! sikulipa bili yangu?" Nilipaswa kukusanya bili.

171 Nikasema, "Loo, ulilipa bili yako. Ninataka kukupa nyingine." Nikasema, "Nina taa hapa."

"Loo, sina uwezo wa kuinunua."

172 "Sasa ngoja kidogo. Sijakuambia uinunue hata kidogo. Nina nyingi tu za hizo, ni—ninataka kuacha moja nyumbani mwako. Iweke tu majuma kadha, na uifurahie, nami nitarudi

na kuichukua. Tunapaswa kutangaza vitu hivi, zichukue tu, kwa hiyo nitaiweka tu nyumbani mwako."

173 "Vema, sasa, Billy, ni—nisingeweza kabisa kuinunua. Sina pesa za kuinunua."

174 "Hata sijakuambia uinunue, sivyo? Nimesema tu ninataka kuacha moja nyumbani mwako, nikuachie uifurahie."

"Si utani?"

175 "Hata kidogo. Unanijua mimi. Nitarudi na kuichukua. Nitaichukua tena katika majuma mawili. Vema. Nitapitia tu hapa na kuichukua. Jambo pekee ninalokutaka ufanye, ni kuninii tu . . . Ninataka kuziondoa kutoka kwenye gari langu, nipate mahali pa kuiweka. Inanibidi kuacha kadha hapa. Ni—ni—ninataka kuziondoa kwenye gari langu. Si—sikukutaka wewe uinunue. Sikukuambia uinunue. Nilikuomba tu uache ikae hapa."

"Vema, na kama ikivunjika je?"

"Hilo ni juu yangu. Mimi ndiye ninayesimamia hilo."

176 Nilijua hiyo taa ingejiuza yenyewe. Nilijua ilikuwa ni bidhaa nzuri. Nikaweka hiyo taa mle nyumbani. Sikurudisha kumi kutoka katika zile mia mbili. Nikashinda shindano lile. Kwa sababu gani? Kwa nini? Hiyo taa ilijiuza. Mara unapoiona, na kuona jinsi ilivyo, basi unaitaka. Itajiuza yenyewe.

177 Ni jambo lile lile. Hatuhitaji kuwa na madhehebu makubwa tupate kumwuza Kristo. Hatuna haja ya kuwa na wahubiri walio na elimu sana, na watu wa hali ya juu sana ambao ni mameya, na vitu mbalimbali vya mjini. Kile tunachopaswa kuwa nacho ni Kristo. Na Kristo hujiuza Mwenyewe. Ukimweka Kristo katika moyo wa mwanadamu, haikulazimu kumwambia, "Unapaswa kujiunga na madhehebu *haya*, ama *yale*." Yeye tayari anaipenda sana hiyo bidhaa.

178 Je! una njaa? "Heri wenye njaa na kiu." Tunakaribia kuja kwenye meza ya Bwana sasa. Kwa wale ambao hawajaninii bado, huenda, hujampokea Kristo maishani mwako . . . Kama wewe ni Mkristo, basi unaona njaa. Nimekuwa Mkristo, miaka thelathini na moja sasa, na kila siku ninamwonea Kristo njaa zaidi kuliko nilivyomwonea wakati nilipoanza. Yeye anakuwa mtamu zaidi siku zinavyoendelea.

179 Nami ninaangalia maskini vibao Vyake vya matangazo, ninapowaona wakipita mtaani, ninawaangalia huku nje hospitalini, ninawaangalia katika saa ya kufa kwao, ninawaangalia huku nje wakati wako kwenye mashindano ya kuamua, ninamwangalia maskini bibi huyo mdogo, jinsi anavyojishikilia pale kama mtakatifu halisi na wa kweli.

180 Nilisimama kwenye kaunta, hapa si muda mrefu uliopita, nikamwangalia bibi mdogo. [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] . . . akagutuka, akageuka. Nikasema, "Je! unamjua Yesu

kama Mwokozi wako?" Na mvulana huyo akainamisha kichwa chake chini, akageuka, mlangoni, unaona, hakuniangalia kamwe. Haya basi. Loo, mwanamke huyo hakunijua, bali nilimjua. Nilimjua. Nikamwangalia. Ameolewa sasa. Ameolewa na maskini mhubiri kijana, naye anaendelea vizuri.

181 Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo, unaona, ninapenda kuangalia ubao huo wa matangazo. Ninapenda kuuangalia. U—unanifanya kuwa na njaa, ninafikia mahali ambapo, hapo, tunaweza kula, kula Chakula cha kiroho. Kwa maana, nilijua msichana huyo hakuwa mshiriki wa kanisa. Alikuwa Mkristo. Hiyo ni kweli. Ndiyo. Unaweza kujua.

182 Biblia ilisema, ingawa...Petro na Yohana, baada ya kumponya yule mtu kwenye lango linaloitwa Nzuri. Alikuwa ni kiwete, tangu tumboni mwa mama yake. Hakuwa na nguvu nyingi. Hangeweza kusimama kwa muda mrefu sana. Ilimbidi Petro kumshikilia, kumfanya atembee, ameponywa. "Tangu tumboni mwa mamaye." Na walipomleta mbele ya ile halmashauri, na kuwakataza kuhubiri katika Jina la Yesu. "Nao wakaona ya kwamba walikuwa hawana elimu," Biblia ilisema. Mitume hawa, Yohana na Petro, walikuwa ni watu wasio na elimu wala maarifa. Hawakujua theolojia yo yote kubwa. Walikuwa wavuvi; hawakuweza kuandika jina lao. Bali walisema, "Iliwabidi kuwatambua hao, ya kwamba walikuwa pamoja na Yesu." Walikuwa ni nini? Vibao vya matangazo, vibao vya matangazo.

183 Loo, tungeweza kuendelea. Mungu, atusaidie tuwe vibao vya matangazo. Jalia Maskani hii ya Branham hapa, mahali hapa padogo palipowekwa wakfu na kutolewa kwa Mungu, jalia patoe vibao vidogo vya matangazo huku nchini kote, ambavyo vitalifanya taifa hili lote lenye njaa na kiu limjie Kristo, ndilo ombi langu.

Na tuinamishe vichwa vyetu kidogo.

184 Baba uliye mwingi wa neema, sisi kweli ni watu waliobarikiwa, kuwa na Kristo maishani mwetu na mioyoni mwetu. Tunashukuru sana kwa ajili Yake, Baba yetu. Tunajua, ya kwamba, kumjua Yeye ni Uzima. Si kujua kanuni ya imani, si kujua Kitabu, bali kumjua Kristo, ni Uzima. Na, Baba Mungu, sisi ambao tumempata Yeye namna hiyo, Mwokozi wetu, mponya wetu, nguvu zetu, msaada wetu, msaada wetu hutoka kwa Bwana. Sisi tunakiri kwamba si kitu; hatujui kitu. Kuna kitu kimoja tu tunachojua ama tunachopenda kujua, ni Kristo, katika nguvu za kufufuka Kwake. Kwa kuwa, kila mtu anayeamini jambo hili, yuna Uzima wa Milele.

185 Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utabariki kanisa hili dogo, na watu hawa walio hapa katika usiku huu wenye joto, katika jioni hii ya Sabato hapa, tukiketi kwenye maskani hii ndogo ya mbao, tukingojea baraka za Mungu.

186 Maneno haya macheche yaliyochanganyikana na yaliyokatika-katika na ufasaha ambayo yamesemwa, kuona njaa, na msafiri kuona ubao wa kuwekea matangazo. Mungu, tufanye wenye njaa sana na wenye kiu, hata tutaangalia vibao Vyako vya matangazo, tuone maisha ya Kikristo. Jalia tuwe vibao vya matangazo kwa ajili Yako. Naomba uakisi Nuru Yako kwa nafsi iliyo na njaa, wapate kuona njaa watakapoona ubao huo wa matangazo tunaotangaza. Kristo, mdhamini wetu, ametupa maisha matulivu ya amani, furaha kamili na nguvu nafsini mwetu, na kuishi maisha ili kwamba watu wangetaka kuwa namna hiyo. Tujalie, Bwana. Tupe maisha hayo sisi sote.

187 Na huenda wakaweko wengine hapa, ambao bado hawajaona jambo hilo, bali usiku wa leo wamekuwa wakijifunza na kuangalia mbele, kote katika safari ya maisha, kwa watakatifu wa kale mbalimbali, hao mama wazee wa siku zilizopita, mtu yule waliyemcheka akiwa kando ya barabara na wakafikiri alikuwa amerukwa na akili, amesimama hapo akihubiri. Lakini sasa wanaona ya kwamba mtu huyo alikuwa ni ubao wa matangazo. Alikuwa ni ishara iliyokuwa ikielekeza. Yule mama mzee aliyetakaswa aliyeshuka kwenda mtaani, akiwa nywele zake zimesokotwa nyuma, [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] na, hata hivyo, sisi vijana huenda tuliwacheka, na kuwazia, "Huyu ni kitu cha kikale cha namna gani?"

188 Bali tunatambua, Bwana, huyo alikuwa ni ubao wa matangazo ya Uzima wa Milele. Tuliupita tu, Baba. Tunasikitika. Tunasikitika. Tujalie turudi na kuanza tena kuufuatia, usiku wa leo, Baba. Tufanye namna hiyo. Tupe Uzima. Tunataka kuonekana kama watakatifu, mbele Zako. Tunataka kutenda namna hiyo. Yule mtu tuliyemnena mabaya, mtu yule tuliyemgombanisha, hakujibu neno, bali alikuwa ni mpole sana, na kusema, "Hilo ni sawa, mwanangu. Bwana akubariki."

Vivyo Hivyo Nuru Yenu na Iangaze Mbele ya Watu SWA61-0903
(Let Your Light So Shine Before Men)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, 03 Septemba, 1961, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 2003 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2003 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org